

SHINGO YA KIZAZI NI NINI?

- ◆ Shingo ya kizazi ‘cervix’ ni sehemu ya kizazi kati ya uke na mji wa mimba. Sehemu hii ina kazi nyingi ikiwemo;
- Kupitisha mbegu za kiume kuelekea katika mji wa uzazi na hatimaye mirija ya uzazi ili kupevusha yai,
- Kupitisha damu ya hedhi
- Mlango anaopitia mtoto wakati wa kuzaliwa.

SARATANI YA SHINGO YA KIZAZI

- ◆ Hii ni aina ya saratani inayoshambulia seli/chembechembe zilizoko ndani ya ngozi laini inayozunguka shingo ya kizazi.

NINI CHANZO CHAKE

- ◆ Husababishwa na aina ya virusi kinachoitwa ‘Human Papilloma Virus’ (HPV), kirusi hiki huambukizwa kwa njia ya kujamiihana na mtu mwenye maambukizi.
- ◆ Kuna tabia au hali hatarishi ambazo zinachangia mtu kupata saratani ya shingo ya kizazi, tabia/vitu hivyo ni

pamoja ana;

- Kuanza ngono katika umri mdogo (chini ya miaka 18).
- Uvutaji wa sigara.
- Kuwa na wapenzi wengi au kujamiihana na mtu mwenye wapenzi wengi.
- Matumizi ya mafuta mengi kwenye chakula au kula vyakula vyenye mafuta kwa wingi.
- Kutokula mboga za majani na matunda.
- Upungufu wa kinga mwilini.

DALILI ZA SARATANI YA SHINGO YA KIZAZI

- ◆ Saratani ya shingo ya kizazi huanza na kuendelea kwa muda mrefu bila kuonesha dalili zozote. Dalili ambazo zinaweza kujitokeza wakati ugonjwa upo katika hatua za mwisho ni pamoja na;
- ◆ Kutokwa na damu isiyo ya hedhi ukeni.
 - Kutokwa na damu ukeni baada ya kujamiihana.
 - Kutokwa na damu ukeni kwa

wanawake waliokwisha kukoma hedhi.

- Damu iliyochanganyikana na majimaji ya uke.
- Matone ya damu au damu kutoka kipindi kisicho cha hedhi.
- ◆ Kutokwa na majimaji au uchafu ukeni wenyewe harufu mbaya wakati mwingine ukiwa umechanganyika na damu.
- ◆ Maumivu wakati wa kujamiihana
- ◆ Maumivu chini ya tumbo, nyonga na kiunoni.
- ◆ Kukojoa mkojo wenyewe damu,
- ◆ Kupitisha mkojo na haja kubwa kwenye uke na
- ◆ Upungufu wa damu.

NAMNA YA KUGUNDUA SARATANI YA SHINGO YA KIZAZI

- ◆ Saratani ya shingo ya uzazi huchukua muda mrefu mpaka kuonesha dalili.
- ◆ Vipimo vya uchunguzi vinavyofanyika ni pamoja na;
 - **Pap Smear** - Kipimo hiki ni rahisi na hakina madhara yoyote. Inashauriwa kufanya kipimo hiki

mara moja kwa mwaka.

- **Colposcopy** - Hiki ni kipimo kinachotumia darubini kuangalia chembechembe/ seli zilizondani ya ngozi inayozunguka shingo ya uzazi.

MATIBABU

- ◆ Matibabu ya saratani hutolewa kulingana na hatua ya ugonjwa.
- ◆ Ugonjwa ukiwa hatua za mwanzo huweza kutibika kabisa (ingawa kuna uvezekano wa kujirudia).
- ◆ Hatua za mwisho za ugonjwa huu huwa haziwezi kupona kabisa. kinachofanyika mara nydingi ni kutoa matibabu yatayotuliza dalili na maumivu na kumuwezesha mgonjwa kuishi vizuri.
- ◆ Huduma za matibabu hutolewa kwa njia zifuatazo:
 - Upasuaji katika hatua za mwanzo za ugonjwa.
 - Mionzi.
 - Dawa za Saratani.
 - Mionzi pamoja na dawa za saratani.

NAMNA YA KUJIKINGA NA SARATANI YA SHINGO YA UZAZI


- ◆ Kupata chanjo ya 'Human Papilloma Virus'.
- ◆ Kuepuka ngono katika umri mdogo.
- ◆ Kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu.
- ◆ Kutumia kondomu kila mara unapojamiiiana.
- ◆ Epuka kuvuta sigara.
- ◆ Kufanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi angalu mara moja kwa mwaka.
- ◆ Tibu kikamilifu magonjwa ya ngono (STI).
- ◆ Punguza matumizi ya mafuta mengi kwenye chakula.



**CHUO KIKUU CHA
DAR ES SALAAM**

KITUO CHA AFYA

S.L.P. 35074
DAR ES SALAAM



SARATANI YA

SHINGO YA KIZAZI

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Kituo cha Afya-Chuo Kikuu cha DSM

Simu: 2410500-8 Ext. 2006

2410014

Barua pepe: healthcentre@udsma.ac.tz

'A Healthy Mind Thrives in a Healthy Body'